**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni** 2024

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu..**

**Mkuu wa Shule 0719703558**

**Makamu Mkuu wa Shule.0623607125**

**Shule ya Sekondari Dinyecha**

**S.L.P. 559**

**MTWARA**

**……/…./2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**.......................................................**
**S.L.P ............................................**
**………………………………..…....**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI DINYECHA, HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA, MKOA WA MTWARA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao………………………………. amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024, na atasoma tahasusi ya HGK/HGL /HGFa

Shule ya Sekondari Dinyecha ipo umbali wa Kilometa 03 Kusini mwa Mji wa Nanyamba Usafiri kutoka mjini Nanyamba unapatikana katika kituo cha mabasi cha Nanyamba nauli ni shilingi 2,000 kwa pikipiki na shilingi 3,000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……………, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

a) Sketi ya rangi ya ugoro linda box ndefu hadi mwisho wa ugoko (jozi moja) Shati nyeupe ya mikono mirefu au nusu kanzu nyeupe zisizobana za mikono mirefu ( jozi moja)
b) Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
c) Sare ya michezo ni trak suit ya bluu na raba nyeupe.(jozi moja)
d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, soksi jozi mbili nyeupe za shule
e) Sweta la rangi ya ugoro;

f) Nguo za kushindia (*shamba dress*) gauni 2 za rangi ya damu ya mzee na mitandio au Majuba ya rangi ya pinki
g) Tai ya rangi ya ugoro
h) Tisheti ya rangi ya ugoro zitapatikana shuleni

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

(i) Madaftari counter book 12 na faili 2
(ii) **Ream (A4)** mbili (02) kwa mwaka;
(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
(iv) Scientific Calculator;
(v) Mashuka jozi 2, rangi ya pink, godoro 1, mto na chandarua 1
(vi) Nguo za ndani za kutosha, taulo ya kuogea na taulo za kike za kutosheleza muhula mzima
(vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
(viii) Ndoo ndogo mbili (02) za lita Kumi zenye mifuniko
(ix) tochi ya kumsaidia umeme ukikatika (taa ya solar isiwe ya kuchaji kwenye umeme)
(x) Kwanja 01, jembe 01, reki 01, mifagio 02 wa ndani na nje.
(xi) Kadi ya mfuko wa matibabu
(xii) Sanduku imara la kuwekea vitu na kufuli lake

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

michango yote ilipwe kupitia benki, **SHULE YA SEKONDARI DINYECHA- 71010040425 NMB,** tawi la Tandahimba

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**MWAJUMA GADDY MNAYAHE**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0719703558**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0623607125/ 0742435878**
- **Mwandamizi Taaluma 0784197209**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To be completed by a medical officer (NAME) ……………………………………………………………………

Name of student……………………………………………………………………………………………………………
Form …………………………………… Term ……………………….. Year ……………………………………

Dear Doctor

Please kindly examine the above named student to prove her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray (     )   2. Urine (    )   3. Stool (  ) 4. Physical fitness  (     )   5. V.D (    )   6. Tuberculosis (     )  7. Pregnancy (     )

A: (I) PRELIMINARY INFORMATION BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)

| NO | DISEASE | YES/NO | NO | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear, Nose and threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serio Accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and Urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder. | |

**(II) VACCINATION AND INNOVULATIONS HISTORY**

| **DISEASE** | **1ST DATE** | **2ND DATE** | **3RD DATE** |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whooping cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow fever | | | |
| Cholera | | | |

**Official**

B: MEDICAL EXAMINATION REPORT

a. weight

b. heart beat

c. vision

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider that she is physically fit/unfit to undergo studies.

DOCTOR'S NAME……………………………SIGNATURE …………… ***(Official stamp)*** …………………..

STATION……………………………DATE ………….…………PHONE……………………………….

**SHULE YA SEKONDARI DINYECHA S. L. P 559. MTWARA**

**TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI MPYA**.

**SEHEMU A.**

JINA LA MWANAFUNZI

………………………………………………………………………………………………………

wa kidato cha ……….. Mchepuo wa …................. Mwaka ………………………………..

Dini …………………………………………………………………………………………………

**ELIMU**

(i) Shule ya Msingi niliyosoma ni …………………………………..……… iliyopo (Kata) ………………………

Wilaya ya …………………………………………………… Mkoa wa …………………………………………

kuanzia mwaka …………………………………………….. mpaka ……………………………………………

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI NA JAMAA:**

(i) Baba anaitwa

………………………………………………………………………………………………………………

Anaishi kijiji/mtaa ………………………………………………………… kata …………………………………

Kazi yake ni …………………………………………………….. na anwani yake ni …………………………

………………………………………………………………………………………………………………

Namba yake ya simu ni

…………………………………………………………………………………………………….

(ii) Mama yangu anaitwa ……………………………………………………………………………………

Anaishi kijiji/mtaa ………………………………………………………… kata …………………………………

Kazi yake ni …………………………………………………….. na anwani yake ni ………………………..

………………………………………………………………………………………………………………

Namba yake ya simu ni ………………………………………………………………………………………

(iii) Jina kamili la Mzazi/Mlezi anayemuhudumia mwanafunzi ikiwemo kumpatia mahitaji yake muhimu

……………………………………………………………………………………………………………….

Uhusiano ………………………………………………………………………………………………………

Anuani Kamili ………………………………………………………………………………………………

Simu ………………………………………………………… Barua pepe …………………………………..

Kazi yake ……………………………………………………………………… Umri ………………………

(iv) Uwepo wa Wazazi: Baba – YUPO HAI/AMEFARIKI. Kama amefariki ni lini? …………………………………

Mama – YUPO HAI/AMEFARIKI. Kama amefariki ni lini? ……………………………………………………..

(v) Majina na picha za watu wasiozidi watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi

| | | |
|---|---|---|
| Jina…………………….. | Jina ……………………….. | Jina …………………….. |
| Uhusiano…………………. | Uhusiano…………………… | Uhusiano ………………. |
| Simu ………………………. | Simu ……………………….. | Simu …………………….. |

Mimi ……………………………………………………………….. ambae ni mwanafunzi wa kidato cha V /VI mchepuo wa ………………………………. katika mwaka wa masomo ………………………….. nathibitisha kuwa maelezo yote niliyoyatoa hapo juu ni ya kweli na sahihi.

**SEHEMU C: UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI**

Mimi …………………………………………………………. nakiri kuwa nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule kwa umakini na utulivu kubwa. hivyo basi ninaahidi “nitazifuata sheria, kanuni na taratibu za Shule kama zilivyoelekezwa. aidha ninaamini kuwa sheria na taratibu zote zipo kwa nia ya kunisaidia katika nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu na taaluma.”

Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu

Jina la mwanafunzi ………………………………………. Sahihi ……………… tarehe…………………………

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………… Sahihi ………………tarehe…………………………

ORODHA YA VITABU AMBAVYO MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO NA SITA ANAPASWA KUJA NAVYO KULINGANA NA MASOMO YA TAHSUSI YAKE

1. **HISTORY**
    - ✞ HISTORY PAPER ONE FOR ADVANCED LEVEL, SALEHE YASIN.
    - ✞ ESSENTIALS IN ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER 2, SALEHE YASINI.
2. **GEOGRAPHY**
    - ✞ KAMILI. 2 (2016) PRACTICAL GEOGRAPHY ALIVE
    - ✞ MSABILA D.T (2018) A COMPREHENSIVE APPROACH TO PHYSICAL GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOL, DAR-ES-SALAAM, TANZANIA
    - ✞ MTEGETWA M. (2001) GEOGRAPHY MAP SHEET PREPARATION FOR ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY SCHOOL EDUCATION EXAMINATION
    - ✞ MSABILA D.T. (2018) AN INTERGRATED REGIONAL STUDY ON HUMAN ANDECONOMIC GEOGRAPHY ADVANCED LEVEL PAPER 2.
3. **KISWAHILI**

    RIWAYA
    - Usiku Utakapokwisha
    - Kufikirika
    - Mfadhili
    - Vuta n'kuvute

    USHAIRI
    - Chungu Tamu
    - Fungate ya Uhuru
    - Mapenzi Bora
    - Kimbunga

    TAMTHILIYA
    - Morani
    - Nguzo Mama
    - Kivuli Kinaishi
    - Kwenye Ukingo wa Thimu

4. **ENGLISH LANGUAGE**
    - ✞ ADVANCED LEVEL ENGLISH: A PRACTICAL APPROACH-NEW EDITION. NICHOLOUS ASHELI
    - ✞ ANALYSIS OF LITERARY WORKS. NYAMBALI NYANGWINE

✦ **Novels** ○ Encounters from Africa – **Macmillan Education Limited**
- The Beautiful Ones Are Not Yet Born – **Ayi Kwei Armah**
- A Man of the People – **Chinua Achebe**
- Divine Providence – Severine **N Nduguru**
- The Rape of the Pearl – **Magala Nyago**
- Vanishing Shadows – **Namige Kayondo**

- His Excellence the Heads of State – **Danny Safo**
- A season of Waiting – **David Omowale**

- **Poetry**
  - Selected Poems – TIE
  - The wonderful surgeon and Other Charles Muloka Poems.

5. **GENERAL STUDY**
   - BIGIRWAMUNGU J. (2010). UNDERSTANDING GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL AFRICA PROPER NETWORK, DAR-ES-SALAAM TANZANIA
   - NYANGWINE C.M. (2018) ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES NOTES FORM 5 & 6 DAR-ES-SALAAM TANZANIA
   - KAMILI Z. (2017) GENERAL STUDIES ALIVE KAMILI BOOKS AND GENERAL SUPPLIES DAR-ES-SALAAM.